# JARIBIO LA MTIHANI WA NANDI

## DARASA LA NANE - MWAKA 2019

## KISWAHILI : LUGHA

**MUDA: SAA 1 DAKIKA 40**

**SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO**

1. Umepewa karatasi hii ya maswali na karatasi ya kujibia. Karatasi hii ina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika karatasi hii
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika KARATASI YA MAJIBU na wala siyo katika karatasi hii ya maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo umeandika katika karatasi ya majibu:

   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**

   **JINA LAKO**

   **JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
9. Kwa kila swali 1 - 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano:-**

**Katika kartasi ya maswali:**

**30. Jaza pengo:** _____ ni mti ambao magome yake hutumia kama viungo katika mapishi.

A. Mdalasini

B. Karafuu

C. Pilipilimanga

D. Iliki

Jibu sahihi ni (A) (**Mdalasini**)

**Katika karatasi ya majibu:**

**16** [A] [B] [C] [D] **22** [A] [B] [C] [D] **25** [A] [B] [C] [D] **30** ~~[A]~~ [B] [C] [D] **35** [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba **30**, kisanduku chenye herufi **A** ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Karatasi hii ina maswali 50 iliyopigwa chapa.**

**FUNGUA UKURASA**

**Chagua jibu lifaalo zaidi kujazia mapengo**

__1__ upweke ni __1__. lakini mimi __2__ kubaki __3__ yangu nyumbani. Wakaa __5__ ndipo nilipong'amua kwamba heri jirani __6__ ndugu wa mbali. Nilitamani __7__ jirani mmoja aje anisaidie lakini wapi! Uchu wangu ulikuwa. __9__ Niliambulia __10__

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Lau | Hata | Seuze | Ingawa |
| 2. | maradhi | uvundo | ndwele | upweke |
| 3. | nililazimika | inanilazimika | ililazimika | alilazimishwa |
| 4. | kipekee | pekupeku | peke | pekee |
| 5. | huo | hao | huyo | hiyo |
| 6. | kumliko | kuzidi | kushinda | kuliko |
| 7. | mbona | punde | angaa | kwani |
| 8. | zake | petu | kwao | kwake |
| 9. | Haupiki haupakui | Bure bilashi | Hauoni hausikii | Alfa na omega |
| 10. | nunge | palipo | chembe | mema |

Bila kupuuza __11__ na juhudi zako, leo ninayo huzuni na __12__ kukufahamisha __13__ kwa mara __14__ mazingira yanachafuliwa. Hili jambo __15__ sana.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 11. | upuuzi | karaha | wajibu | athari |
| 12. | jitimai | raha | jozi | furaha |
| 13. | kua | kwamba | licha | lau |
| 14. | ingine | mengine | jingine | nyingine |
| 15. | limenitia moyo | limenipiga moyo konde | limenivunja moyo | limenitia upondo |

**Kutoka swali la 16 hadi 30, jibu kulingana na maagizo**

16. Chagua neno ambalo ni kisawe cha kibali
    A. Risiti B. Ruhusa
    C. Stakabadhi D. Shahada

17. Chagua kinyume cha sentensi hii
    **Nina furaha kwa kuungana na shaibu.**
    A. Sina raha kwa kutoungana na bikizee.
    B. Nina huzuni kwa kutangamana na ajuza.
    C. Nina majonzi kwa kutengana na ajuza.
    D. Sina jitimai kwa kutotangamana na shaibu

18. Chagua umoja wa sentensi ifuatayo.
    **"Mawe mazuri na matunda mabaya ni yetu".**
    A. Jiwe zuri na tunda baya ni langu.
    B. Tunda baya na jiwe nzuri ni yangu.
    C. Jiwe nzuri na tunda mbaya ni yangu.
    D. Tunda zuri na jiwe mbaya ni langu.

19. Kanusha katika wingi wa ukubwa.
    **Uso wa mama umeiva kwa kulia.**
    A. Vijuso vya vimama havikuiva kwa kulia.
    B. Majijuso ya majimama hayataiva kwa kulia
    C. Majusoya majimama hayajaiva kwa kutolia.
    D. Vinyuso vya kina mama haviivi kwa kutolia

20. Sahani na______ni kama chungu na mkungu.
    A. kikombe B. kawa
    C. sinia D. kijiko

21. Chagua methali inayofaa maelezo haya.
    <u>**Tumejaribu kulilia wabunge wetu wasijiongeze mishahara lakini wametupuuzilia mbali.**</u>
    A. Nyani haoni kundule, huona la mwenziwe.
    B. Dua ya kuku haimpati mwewe.
    C. Kila chombo kwa wimbile.
    D. Apendwaye akijua, hujishaua.

22. Ukinichora mimi ni kama umbo la mkate. Mimi ni________
    A. tao B. kiegema
    C. hori D. mche duara

23. **1,3,5,6,9,15**. Nambari hizi huitwa?
    A. Kipeo B. Shufwa
    C. Witiri D. Tasa

24. Neno waya huwa katika ngeli ya_
    A. U -ZI B. I - ZI
    C. U -1 D. A - WA

25. Kihisishi gani kinachoonyesha dharau?
    A. Olewangu! B. Ebo!
    C. Masalaale! D. Sadakta!

26. Chagua jawabu lenye kinyume cha kitenzi.
    A. Mrefu - mfupi B. Haraka - taratibu
    C. Kwetu - Kwao D. Beba - Tua

27 Kitate cha neno panda ni__________
    A. shuka B. kwea
    C. banda D. pandisha

28. Malipo ya awali ya kufunga kitu unachotaka kununua ni__________.
    A. ushuru B. arbuni
    C. karadha D. kifungua mkoba

29. Chagua sentensi iliyo katika wingi wa nafsi ya pili
    A. Nyinyi mna mazoea yasiyopendeza.
    B. Wao hawana haraka maishani.
    C. Sisi tunayasoma masomo magumu.
    D. Wewe hukupewa mwaliko maalum

30. Kuharibu kile ambacho hukunufaisha sana ni____________
    A. kumeza mrututu
    B. kujitia hamnazo
    C. kupiga vijembe
    D. kutia kitumbua mchanga

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31- 40.**

Mwenzangu keti nikujuze juu ya maendeleo ya vitongoji vya kwetu. Katika Jamhuri va Sadikika watu wanalshi. Pamoja kijijini.

Walianzisha vijiji hivi kwa ajili ya kuondoa dhuluma na dhiki ya mambo mengi ya lazima, na kwa maisha bora na ustawi. Wanaishi kwa jasho lao. Utangamano ndio ngome na msingi wa maendeleo. Watu wa kila janibu na katika vitongoji vya nchi nzima wote ni kama ndugu. Wote wanaishi kwa umoja. Ubaguzi umekwisha zikwa kwenye kaburi la sahau. Wote wanapenda kazi zaoza kilimo. Hakuna anayepinga maendeleo. Ni aibu kwa mwana kijiji kulazadamu. Shibe ndio ngao yao.

Kila mmoja anapigana jino na ukucha kujaribu kuondoa hali ya unyonge, ufukara, ukosefu na hasa kwa kuleta haraka iwezekanavyo hali ya maendeleo na ustawi kwa nchi nzima ya Sadikika.

Mapato ndiyo matumaini yao. Buni, chai, mkonge, karanga, mananasi, mboga, vitunguu, kunde na kadhalika ndiyo mazao yalimwayo maridhawa nchini kote. Wanavijiji wanafuata vyema mashauri na maongozi yote yanayotolewa na chama cha wakulima au mabwana shamba. Mbolea na dawa za kuua wadudu zinatumika. Njia mpya na vyombo vya kisasa vinatumika. Pia mapato ya kijiji hutumika kuanzisha na kuendeleza mipango ya ufugaji, mambo ya starehe, shule, hospitali, simu na posta misikiti, makanisa, maji, maduka na ushirika na huduma nyinginezo. Pia kila kijiji kimejaribu kutengeneza barabara safi.

Maduka ya wanavijiji yanaondoa dhuluma ya kunyonywa na wachache. Hakuna awezaye kudai au kuliita duka fulani ni lao. Duka lote ni la ndugu wote, wana wa janibu. Kila duka lina kijana aliyehitimu hesabu vizuri. Kwa kuwa yeye ni mjuzi wa hesabu, ndiye aliyechaguliwa kuwa mweka hazina wa duka hilo. Na kila mwisho wa mwezi kijana huyu hutoa taarifa yake ya fedhi kwa halmashauri ya kijiji.

Mapato ya kilimo na mapato ya duka hugawanywa kwa kufuata utaratibu uliokubaliwa. Viongozi na hata watumishi wa serikali hawaingilii sana vijiji hivi ila ikiwa kuna tatizo kubwa. Hata hivyo viongozi wa serikali wanaangalia kuona kwamba watu wote wanapata chakula bora, na hasa watoto kunywa maji safi ili kuepukana na magonjwa, kutoa huduma kwa akina mama, kuendeleza afya ya watu kwa jumla.

31. Katika Jamhuri ya Sadikika watu wanaishi
    A. kwa jasho lao
    B. kwa mpango maalum
    C. kwa jasho la wenzao
    D. kwa shibe, siyo ngao

32. Badala ya kutumia neno maridhawa mwandishi angeweza kutumia:-
    A. Kwa kiasi tu B. Kwa jumla
    C. Tele D. Kwa uchache

33. Madhumuni ya kuanzisha vijiji katika Jamhuri ya:-
    A. Kuondoa dhuluma, dhiki na ubora wa maisha.
    B. Kuondoa dhiki pamoja na ubora wa maisha
    C. Kuondoa shida pamoja na maisha bora na ustawi
    D. Kuondoa taabu maishani na kustawisha maisha

34. Kulingana na taarifa, unyonyaji unaletwa na
    A. faida za biashara, kuendeleza sehemu zote za vijiji
    B. biashara kumilikiwa na wachache
    C. mapato kugawanywa kwa kotofuata utaratibu
    D. duka lote kuwa la ndugu wote wajanibu

35. Wanasadikika wote ni __________
    A. wakulima na wafanyakazi
    B. wafitini na wanyinyaji
    C. wazalendo na wanatangamana
    D. wakulima na wazazi

36. Wanasadikika waliamua kujiunga pamoja na kuondoa
    A. ufukara B. maradhi
    C. ubepari D. ujinga

37. Methali ambayo ni ya kukazia habari hii ni:-
A. Subira huvuta heri
B. Usisahau baharia kwa sababu ya unahodha
C. Suluhu haiji ila kwa ncha ya upanga
D. Umoja ni nguvu utengamano ni udhaifu

38. **"Kulaza damu"** limetumika katika taarifa. maana
A. kutolegeza juhudi ya maendeleo
B. kulegeza juhudi
C. kutia bidii zaidi
D. kutia fora

39. Jukumu kubwa la kazi ambalo linawakabili watumishi wa serikali kijijini ni?
A. Kuchangia hazina ya maendeleo kijijini
B. Kuingilia na kutoa mwongozo wa kazi kwa wanakijiji
C. Kuimarisha kilimo kijijini
D. Kuangalia kama huduma za afya, maji na chakula zinaendelea vilivyo

40. Kupigana kwa jino na ukucha ni
A. kukaa imara
B. kupatwa na jabazi
C. kupigana kwa bidii zote
D. kujitoa uvivu

**Soma habari ifuatavo kisha ujibu maswali 41- 50.**

Safari ilikuwa ndefu. Hawakuwa na budi kuenda masia kwa sababu licha ya magari kuadimika kama barafu ya kukaanga, hapakuwa na tariki. Kulikuwa na vijia msituni ungedhani vilitengenezewa panya.

Msitu ule ulikuwa umejaa wanyama tumbitumbi tena wa kila aina. Ilikuwa nadra sana kumwona mtu akitembea peke yake. Yamkini waliamini kuwa kifo cha wengi ni arusi. Wanaume kwa wanawake walikuwa kwenye charo. Walikuwa wakigura sehemu ile kwa sababu walihofia kuvamiwa na wanyamapori. Kila walipopanda mazao yao yalikuwa chakula cha tembo, mbogo na wanyama ambao hula mazao ya shambani. Usiku ulikuwa wa kutisha. Hawakupata hata lepe la usingizi kwa sababu mifugo yao ilikuwa katika hatari ya kushambuliwa na chui, duma na simba. Masaibu yaliwasibu na kuwazingira. Wakaamua kuacha migunda yao ingawa ilikuwa na rutuba ya kupigiwa mfano.

Wanaume waliangata mizigo yao nao wanawake waliitwika. Watoto walielekea na safari ikauma mchanga alfajiri na manyera huku umande ukiwalowesha. Jua liliangaza lakini ukali wamiale yake haikuwasumbua. Safari ilipoanza kunoga ghafla bin vuu, walikifumania kikundi cha mbogo. Mbogo hawa walikuwa wakinywa maji. Bila kuboronga wasaa nyati waliwakabili vilivyo. Kila mtu alitundika guu begani. Ulikuwa wajibu wa mtu kuyaokoa maisha yake. Vumbi lilitifuliwa. Walipoona maji yamezidi unga, walikwea juu ya miti. Nyati walipita wangu wangu na hatua chache baadaye, walikutana na simba. Simba waliamini kuwa mlo umejipeleka wenyewe. Mbogo wa kwanza alishikwa na kutoa sauti ya kutisha. Vita kamili vilizuka dhidi ya simba na nyati. Simba alipambana na kujipatia shibe ilhali nyati alikuwa na nia ya kuyanusuru maisha yake. Katika shamrashamra hizo, nyati walikimbia wakifuatwa kwa kasi na simba.

Hatimaye wasafiri walipata muda wa kuendelea na safari yao. Walikuwa wachovu kupindukia na wenye jitimai. Siku ilianza kukuchwa na hawakuwa na makao maalum ya malazi. Iliwalazimu kuwasha moto mkubwa na kutengeneza malazi karibu na moto huo. Sehemu ile haikuwa na wanyama. Miti ilikuwa mifupi. Ilibidi kutembea kwa muda mrefu iii kupata mvua. Mvua iliponyesha ilikuwa ya kuondoa vumbi tu. Mimea ilinawiri kwa muda kisha ikakaushwa na jua lililoleta joto ungedhani ni tanuri.

41. Si kweli kuwa

A. Baraste zilikuwa nyingi.

B. Vijia vidogo vidogo vilitumika

C. Safari ilikuwa ndefu

D. Kulikuwa na uhaba wa magari

42. Kisawe cha **"Kuenda masia"** ni

A. kuenda chemba

B. kupigamilundi

C. kuenda kwa mesiya

D. kupigamiluzi

43 Wasafiri walisafiri kwa makundi ili

A. kuandamana B. kuhofiana

C. kuhimizana D. kulindana

44. Maana ya neno charo ni

A. kundi la wanyama pori.

B. kuhama

C. kundi la wasafiri.

D. msafarawa ng'ombe.

45. Wasafiri walipata nafasi ya kuendelea na safari wakati

A. kulipokucha

B. nyati walipokimbizwa na simba unyounyo.

C. walipofumania mbogo wakinywa maji.

D. umande ulipohinikiza nyasini

46. Watu walihofia nini hasa ndiposa wakagura?

A. Mvua kupungua kwa kiasi kikubwa.

B. Mmomonyoko wa udongo ulizorotesha rotuba

C. Kushambiiliwa na wanyamapori kila mara.

D. Wanyamapori walianza kula wapita njia

47. **"Walikuwa wachovu kupindukia na wenye jitimai."** Maana

A. Walikuwa na mavune na majonzi ya kutwa.

B. Walikuwa wakihofia wanyamapori usiku

C. Walikuwa na makao maalum ndiposa walichoka.

D. Walikaribia kufika walikokuwa wakihamia.

48. Sentensi ipi inayoonyesha sababu kamili iliyowafanya watu wakose usingizi usiku?

A. Mazao ya mashamba yalikuwa finyu.

B. Uchovu wa kutembea muda mrefu.

C. Hawakuwa na vitanda

D. Iliwapasa walinde mifugo yao.

49. **Simba waliamini kuwa shibe imejipeleka yenyewe**, ina maana :-

A. Wanyamapori wengine walikuwa shibe ya shimba.

B. Walitegemea masiya safarini.

C. Walitembea kwa miguu.

D. Walikuwa wameshiba kutokana na shibe.

50. Vita vilizuka dhidi ya simba na mbogo. Je, ni methali gani ingetumiwa kudhihirisha haya?

A. Vita vya panzi furaha ya kunguru.

B. Hasira ya mkizi furaha ya mvuvi.

C. Angurumapo simba mcheza ni nani?

D. Meno ya mbwa hayaumani.